



Barnebøker for Norge

barnebokser.no

Magozwe / Magozwe

Skrevet av: Lesley Koyi

Illustrert av: Wiehan de Jager

Oversatt av: Lauwo George, Monica Shank Lauwo
(sw), Espen Stranger-Johannessen (nb)

Denne fortellingen kommer fra African Storybook (africanstorybook.org) og er videreformidlet av Barnebøker for Norge (barnebokser.no), som tilbyr barnebøker på mange språk som snakkes i Norge.


Dette verket er lisensiert under en Creative Commons

[Navngivelse 4.0 Internasjonal Lisens.](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/deed.no)

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/deed.no>

Magozwe

Magozwe



✎ Lesley Koyi

👤 Wiehan de Jager

📖 Lauwo George, Monica Shank Lauwo

🗨️ swahili / bokmal

📊 nivå 5

(uten bilder)






Kwenye jiji la Nairobi lenye pilikapilika nyingi, mbali na malezi ya nyumbani, paliishi kikundi cha wavulana wasiokuwa na makwao. Waliipokea kila siku ijayo kama ilivyo. Siku moja asubuhi, walikuwa wanakusanya virago vyao baada ya kulala kwenye baridi kando ya barabara. Ili kuondoa baridi, walikoka moto kwa kutumia takataka. Miongoni mwa kikundi hicho cha wavulana alikuwepo Magozwe. Alikuwa ni mdogo kuliko wote.

...

I den travle byen Nairobi, langt fra det trygge livet hjemme, bodde det en gjeng hjemløse gutter. De tok hver dag akkurat som den kom. En morgen pakket guttene sammen mattene sine etter at de hadde sovet på det kalde fortauet. For å fordrive kulden lagde de et bål av søppel. En av guttene i gjengen var Magozwe. Han var den yngste.



Wakati wazazi wa Magozwe walipofariki, alikuwa na miaka mitano tu. Alienda kuishi na mjomba wake. Mjomba hakumjali Magozwe. Hakumpa chakula cha kutosha. Alimfanyisha kazi nyingi nzito.

...


Da Magozwes foreldre døde, var han bare fem år. Han dro for å bo med onkelen sin. Denne mannen brydde seg ikke om barnet. Han ga ikke Magozwe nok mat. Han tvang gutten til å jobbe hardt.



Magozwe alipolalamika au kuuliza, mjomba wake alimpiga. Magozwe alipouliza kama ataweza kwenda shule, mjomba wake alimpiga na kumwambia, "Wewe ni mjinga, hutaweza kujifunza chochote." Baada ya miaka mitatu ya kunyanyaswa, Magozwe alitoroka kwa mjomba wake. Akaanza kuishi mtaani.

...


Hvis Magozwe klagde eller stilte spørsmål, slo onkelen hans ham. Når Magozwe spurte om han kunne gå på skolen, slo onkelen hans ham og sa: "Du er for dum til å lære noe som helst." Etter tre år med denne behandlingen rømte Magozwe fra onkelen sin. Han begynte å bo på gata.



Magozwe alikuwa amekaa uani kwenye nyumba yenye paa la kijani, akisoma kitabu cha hadithi cha shule. Thomas alikuja na kukaa kando yake. "Hadithi inahusu nini?" Thomas akauliza. "Inahusu mvulana aliyekuja kuwa mwalimu," Magozwe akajibu. "Jina lake ni nani?" akauliza Thomas. "Jina lake ni Magozwe," Magozwe akasema kwa tabasamu.

...

Magozwe satt på tunet ved huset med det grønne taket og leste en barnebok fra skolen. Thomas kom og satte seg ved siden av ham. "Hva handler fortellingen om?" spurte Thomas. "Den handler om en gutt som blir lærer", svarte Magozwe. "Hva heter gutten?" spurte Thomas. "Han heter Magozwe", svarte Magozwe med et smil.



Maisha ya mtaani yalikuwa magumu na wavulana wengi walipambana kila siku ili wapate chakula tu. Mara nyingine walikamatwa, mara nyingine walipigwa. Walipougua, kulikuwa hakuna mtu wa kuwasaidia. Kikundi kilitegemea hela ndogo ndogo walizopata kwa kuomba omba, na kwa kuza plastiki na vitu kukuu. Maisha yalikuwa magumu zaidi hasa kwa sababu ya vita dhidi ya vikundi pinzani vilivyotaka kudhibiti baadhi ya maeneo ya jiji.

...

Livet på gata var vanskelig, og de fleste guttene slet hver dag bare for å finne mat. Noen ganger ble de arrestert, andre ganger ble de slått. Når de ble syke, var det ingen som kunne hjelpe dem. Gjengen var avhengig av de få pengene de fikk fra å tigge og fra å selge plast og annet til resirkulering. Livet var enda vanskeligere på grunn av slasskamper med rivaliserende gjenger som ville ha kontroll over deler av byen.



Magozwe alianza shule na ilikuwa ngumu. Alikuwa na mengi ya kujifunza. Mara nyingine alitaka kukata tamaa. Lakini aliwaza kuhusu rubani na mcheza mpira kwenye vitabu vya hadithi. Kama wao, hakukata tamaa.

...


Magozwe begynte på skolen, og det var vanskelig. Han hadde mye å ta igjen. Av og til ville han gi opp. Men han tenkte på piloten og fotballspilleren i barnebøkene. Som dem ga han ikke opp.



Siku moja Magozwe alipokuwa anachakura kwenye mapipa ya takataka, alikuta kitabu cha hadithi kilichokuwa kimechakaa. Aliondoa uchafu kwenye kitabu na kukiweka ndani ya mfuko wake. Kila siku baada ya hapo, alikitoa kitabu na kuangalia picha. Hakujua kusoma maandishi.

...


En dag mens Magozwe lette i noen søppelbøtter, fant han en gammel fillete barnebok. Han fjernet møkka fra den og la den i sekken sin. Hver påfølgende dag tok han ut boka og så på bildene. Han visste ikke hvordan han skulle lese ordene.



Kwa hiyo Magozwe alihamia kwenye chumba katika nyumba yenye paa la kijani. Alikaa chumba kimoja na wavulana wengine wawili. Kwa ujumla kulikuwa na watoto kumi walioishi kwenye nyumba ile. Waliishi pamoja na Shangazi Cissy na mume wake, mbwa watatu, paka mmoja, na mbuzi aliyezeeka.

...

Dermed flyttet Magozwe inn i et rom i et hus med grønt tak. Han delte rommet med to andre gutter. Til sammen var det ti barn som bodde i det huset. Sammen med tante Cissy og mannen hennes, tre hunder, en katt og en gammel geit.



Picha zilikwa zinaongelea hadithi ya mvulana ambaye alikuja kuwa rubani. Magozwe aliota kuwa rubani. Mara nyingine alifikiria kwamba yeye ni yule mvulana kwenye hadithi.

...


Bidene fortalte fortellingen om en gutt som vokste opp til å bli pilot. Magozwe pleide å dagdrømme om å bli pilot. Noen ganger innbilde han seg at han var gutten i fortellingen.



Alimshirikisha Thomas juu ya hofu aliyokuwa nayo. Baada ya muda Thomas alimhakikishia kwamba maisha yatakuwa bora huko sehemu mpya.

...


Han snakket om det han var redd for med Thomas. Med tiden forsikret mannen gutten om at livet kunne bli bedre på det nye stedet.



Kulikuwa na baridi na Magozwe alikuwa amesimama barabarani akiomba omba. Mtu alimkaribia. "Hujambo? Naitwa Thomas. Nafanya kazi karibu na hapa, mahali unapoweza kupata kitu cha kula," mtu yule alisema. Alionyesha nyumba ya njano yenye paa la buluu. "Natumaini utaenda pale kupata chakula kidogo?" Thomas aliuliza. Magozwe alimwangalia yule mtu, kisha akaiangalia ile nyumba. "Labda," akasema, halafu akaondoka.

...


Det var kaldt og Magozwe stod langs veien og tigget. En mann gikk bort til ham. "Hei, jeg heter Thomas. Jeg bor i nærheten, på et sted der du kan få deg noe å spise", sa han og pekte på et gult hus med blått tak. "Jeg håper du drar dit for å få deg litt mat?" spurte han. Magozwe så på ham, og deretter på huset. "Kanskje", sa han og gikk.



Magozwe alifikiria kuhusu sehemu hii mpya, na kuhusu kwenda shule. Itakuwaje kama mjomba wake alikuwa sahihi kwamba alikuwa mjinga kiasi cha kutoweza kujifunza chochote? Itakuwaje kama watampiga sehemu hii mpya? Aliogopa. "Labda ni heri kuendelea kuishi mtaani," aliwaza.

...


Magozwe tenkte på dette nye stedet og på å gå på skolen. Hva om onkelen hans hadde rett og han var for dum til å lære noe? Hva om de slo ham på dette nye stedet? Han var redd. "Kanskje det er bedre å bo på gata", tenkte han.



Miezi iliyofuata, wavulana wale wa mtaani walizoea kumwona Thomas hapa na pale. Alipenda kuzungumza na watu, hasa walioishi mitaani. Thomas alisikiliza simulizi za maisha ya watu. Alikuwa makini na mwenye subira, na hakuwa na kiburi wala dharau. Baadhi ya wavulana walianza kwenda kwenye ile nyumba ya njano na buluu ili kupata chakula cha mchana.

...

I mangedene som fulgte ble de hjemløse guttene vant til å se Thomas. Han likte å snakke med folk, spesielt de som bodde på gata. Thomas hørte på fortellinger om livene til folk. Han var seriøs og tålmodig, aldri frekk eller respektløs. Noen av guttene begynte å dra til det gule og blå huset for å få mat midt på dagen.



Mnamo mwaka wa kumi wa kuzaliwa kwa Magozwe, Thomas alimzawadia kitabu cha hadithi. Ilikuwa ni hadithi inayohusu mvulana wa kijijini aliyekuja kuwa mcheza mpira maarufu. Thomas alimsomea Magozwe hadithi hiyo mara nyingi, mpaka siku moja akasema, "Nafikiri wakati umewadia wa kwenda shule kujifunza kusoma. Unaonaje?" Thomas alieleza kwamba anajua sehemu ambayo watoto wanaweza kuishi na kwenda shule.

...


Omrking Magozwes tiende fødselsdag ga Thomas ham en ny barnebok. Det var fortellingen om en landsbygut som vokste opp til å bli en berømt fotballspiller. Thomas leste den fortellingen for Magozwe mange ganger, helt til han en dag sa: "Jeg synes det er på tide at du går på skolen og lærer å lese. Hva synes du?" Thomas forklarte at han visste om et sted hvor barn kunne bo og gå på skole.



Magozwe alikuwa amekaa kando ya barabara akiangalia kitabu chake cha picha Thomas alipokaa pembeni mwake. “Hadithi hiyo inahusu nini?” Thomas akauliza. “Inahusu mvulana aliyekuja kuwa rubani,” Magozwe akajibu. “Jina lake ni nani?” Thomas akauliza. “Sijui, siwezi kusoma,” Magozwe akasema kwa sauti ya chini.

...

Magozwe satt på fortauet og kikket i bildeboka da Thomas kom og satte seg ved siden av ham. “Hva handler fortellingen om?” spurte Thomas. “Den handler om en gutt som blir pilot”, svarte Magozwe. “Hva heter gutten?” spurte Thomas. “Jeg vet ikke, jeg kan ikke lese”, svarte Magozwe lavt.



Walipokutana, Magozwe alianza kumsimulia Thomas maisha yake. Alimwelezea kuhusu mjomba wake na sababu zilizomfanya atoroke. Thomas hakuongea sana, wala hakumwambia Magozwe nini cha kufanya, bali alisikiliza kwa makini kila mara. Wakati mwingine waliongea wakiwa wanakula kwenye ile nyumba yenye paa la buluu.

...

Da de møttes, begynte Magozwe å fortelle sin egen historie til Thomas. Det var historien om onkelen hans og hvorfor han rømte hjemmefra. Thomas snakket ikke mye, og han sa ikke til Magozwe hva han skulle gjøre, men han lyttet alltid oppmerksomt. Noen ganger snakket de sammen mens de spiste i det gule huset med det blå taket.